# CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU TANZANI (THTU)

# ANDIKO KUHUSU UUNDAJI NA UENDESHAJI WA MABARAZA YA WAFANYAKAZI MAHALA PA KAZI

**Limetayarishwa na:**
Salum Hamisi,
Afisa Elimu kwa Wafanyakazi
THTU
**MACHI, 2025**

**YALIYOMO**

YALIYOMO ...........................................................................................................i

1. UTANGULIZI..........................................................................................................1

2. MAANA NA MALENGO YA BARAZA LA WAFANYAKAZI ...........................................1

2.1 Malengo ya Baraza la Wafanyakazi ...........................................................2

3. CHIMBUKO NA MSINGI WA KISHERIA WA MABARAZA YA WAFANYAKAZI TANZANIA 2

4. UTARATIBU WA UENDESHAJI WA MABARAZA YA WAFANYAZI (MUUNDO, KAZI, VIKAO, VENUE, MUDA) .......................................................................................3

4.1 Baraza la Wafanyakazi (Campus - Level Council) ...........................................4

4.2 Baraza Kuu la Wafanyakazi (Institution - Wide Council)....................................5

4.3 Mchakato wa Uundaji wa Mabaraza ya Wafanyakazi .......................................7

4.4 Utaratibu wa kuunda Mabaraza ya Wafanyakazi Mahala Pa kazi kwenye Vyama Viwili vya Wafanyakazi ...........................................................................8

4.4.1 Muundo wa Baraza Mseto (Vyama Viwili na Menejimenti ya Taasisi) ........10

4.4.2 Changamoto za mabaraza yanaundwa na Vyama Viliwili vya Wafanyakazi 11

4.5 Orodha ya matawi ya THTU yenye Mabaraza ya Wafanyakazi/Baraza Kuu la Wafanyakazi ...............................................................................................11

4.6 Matawi yanayopaswa kuwa na Baraza Kuu la Wafanyakazi ............................13

4.6.1 Ushauri na Mapendekezo ...........................................................................14

4.7 Kazi/Majukumu za Baraza la Wafanyakazi ....................................................14

5. CHANGAMOTO YA UENDESHAJI WA MABARAZA YA WAFANYAKAZI.....................15

6. MAPENDEKEZO YA UTATUZI WA CHANGAMOTO YA UUNDAJI WA MABARAZA YA WAFANYAKAZI.........................................................................................................15

7. HITIMISHO ..........................................................................................................16

8. REJEA..................................................................................................................17

## 1. UTANGULIZI

Baraza la Wafanyakazi ni miongoni mwa mbinu inayotumika kuakisi/kutekeleza dhana nzima ya ushirikishwaji mahala pa kazi (Workers' Participation). Ifahamike kwamba ushirikishwaji wa Wafanyakazi ni suala muhimu katika kujenge mahusiano mazuri kazini, kuongeza tija ya Taasisi pamoja na kukuza morali ya Wafanyakazi. Hata hivyo katika ulimwengu wa kazi mbinu nyingine za ushirikishwaji ni pamoja na Majadiliano ya Pamoja (Collective Bargaining), Kamati za Pamoja (Joint Committee) pamoja na Board Representation (Bodi) n.k.

Ushirikishwaji Mahala Pa kazi ni hali ya Wafanyakazi kushirikishwa katika mchakato wa maamuzi ya taasisi, hasa katika maeneo yanayoathiri kazi yao, ustawi wao, na utendaji wa jumla wa Taasisi.

Kwa kuzingatia umuhimu wa ushirikishwaji wa wafanyakazi katika maamuzi, ni dhahiri kwamba Baraza la Wafanyakazi lina nafasi kubwa katika kuleta mabadiliko chanya ndani ya taasisi. Ni wajibu wetu sote kuhakikisha kuwa mabaraza haya yanaanzishwa na yanafanya kazi kwa ufanisi ili kufikia malengo ya pamoja na kuimarisha ustawi wa wafanyakazi na taasisi kwa ujumla.

## 2. MAANA NA MALENGO YA BARAZA LA WAFANYAKAZI

**Baraza la Wafanyakazi** ni jukwaa linalotoa fursa ya kuwakutanisha pamoja wawakilishi wa wafanyakazi pamoja na menejimenti ya Taasisi kwa ajili ya kujadili na kushauriana masuala yahusuyo sera na mipango ya taasisi, nia ikiwa ni kuongeza tija. Kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Mahusiano kazini Sura 366 Chama cha wafanyakazi kina nafasi kubwa katika kukamilisha mchakato wa uundwaji wa baraza la wafanyakazi mahala pa kazi.

Ikumbukwe kuwa, baraza la wafanyakazi linaundwa kati ya Mwajiri na Chama cha Wafanyakazi kinachotambulika kama wakala wa majadiliano ya pamoja mahala pa kazi.

## 2.1 Malengo ya Baraza la Wafanyakazi

Baraza la Wafanyakazi lina malengo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na:

i. **Kuwezesha Ushirikishwaji wa Wafanyakazi**: baraza hutoa jukwaa kwa wafanyakazi kushiriki katika maamuzi yanayohusu kazi na maendeleo ya Taasisi.

ii. **Kuboresha Mawasiliano Kati ya Waajiri na Wafanyakazi**: linasaidia katika kuimarisha maelewano na kushughulikia changamoto mbalimbali kazini.

iii. **Kusimamia na Kulinda Haki za Wafanyakazi**: linasaidia kuhakikisha kuwa haki za wafanyakazi, kama vile maslahi ya mshahara, usalama kazini, na mazingira mazuri ya kazi, zinalindwa.

iv. **Kutatua Migogoro ya Kazi kwa njia ya majadiliano**: baraza hutumika kama njia ya awali ya kutatua migogoro kabla ya kufikia hatua za mizozo rasmi.

v. **Kuboresha Mazingira ya kazi na ufanisi wa Taasisi**: linahimiza sera na mbinu bora za kazi ili kuongeza tija na ufanisi wa kazi.

## 3. CHIMBUKO NA MSINGI WA KISHERIA WA MABARAZA YA WAFANYAKAZI TANZANIA

Historia inaturejesha hadi mwaka 1970 ambapo ulitoka Waraka uliotoa maelekezo ya uanzishaji wa Mabaraza ya Wafanyakazi kwenye Mashirika ya Umma ikiwa ni tamko alilolitoa Mwl. Julius Nyerere (Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) wakati wa uzinduzi wa kiwanda cha Friendship Textile Mill, pamoja na mambo mengine alielekeza kuwa Shirika lolote la Umma lenye Wafanyakazi kuanzia kumi (10) na kuendelea linatakiwa kuunda baraza la Wafanyakazi kwa ajili ya Wafanyakazi kushirkishwa katika kupanga, kutekeleza, na kutathmini shughuli za Taasisi lengo likiwa kuongeza tija.

Pamoja na Waraka huo, zipo Sheria mbalimbali zinazotoa muongozo wa uundaji wa uendeshaji wa Mabaraza ya Wafanyakazi nchini Tanzania kama ifuatavyo:

| Na. | SHERIA/KANUNI | KIFUNGU | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 1. | Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Sura 366 | 73 | Chama cha Wafanyakazi kinachotambuliwa kinaweza kufikia makubaliano ya kuanzisha jukwaa kwa ajili ya Wafanyakazi kushirikishwa. |
| 2. | Sheria ya Majadiliano ya pamoja katika Utumishi wa Umma Sura 105 | 30(1) | Kutakuwa na kuanzishwa kwa madhumuni ya ushiriki wa watumishi wa umma katika utekelezaji wa shughuli za umma, **Baraza Kuu la Wafanyakazi**. |
| | | 30(3) | Licha ya masharti ya kifungu kidogo (1), kila Wizara, Idara Huru, Kanda, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi za Serikali na Wakala wa Utendaji wataanzisha **Baraza la Wafanyakazi** kwa njia ambayo Waziri ataweka kwa kanuni. |
| 3. | Kanuni za Majadiliano ya pamoja katika Utumishi wa Umma za mwaka 2003 (T.S. Na. 19) | Sehemu ya IV & V | Imebainisha masuala muhimu kuhusu uendeshaji wa Baraza la Wafanyakazi na Baraza Kuu la Wafanyakazi ikiwa pamoja na muundo, uchaguzi wa Mwenyekiti na Katibu, muda wa kuhudumu, Majukumu ya Baraza, akidi n.k. |
| 4. | Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2022 (T.S. Na. 444). | Kanuni ya 107 | Ushiriki wa Watumishi wa Umma katika majadiliano na maamuzi yanayohusu ustawi wao wa ajira utafanyika kupitia Mabaraza ya Wafanyakazi na mazungumzo kwa mujibu wa Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma Sura 105 |

## 4. UTARATIBU WA UENDESHAJI WA MABARAZA YA WAFANYAZI (MUUNDO, KAZI, VIKAO, MUDA)

Uendeshaji wa mabaraza ya Wafanyakazi nchini Tanzania unafanyika kwa mujibu wa Sheria na Kanuni tajwa hapo juu. Kwa kuzingatia wigo na ukubwa ya Taasisi, baraza linaweza kuwa katika muktadha ufuatao ili kukidhi mahitaji ya Taasisi husika:

i. Baraza Kuu la Wafanyakazi (Master Workers' Council)
ii. Baraza la Wafanyakazi (Workers' Council)

Kwa hiyo, katika kuongeza tija ya utekelezaji wa dhana ya Wafanyakazi kushirkishwa katika eneo la kazi, mathalani Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania katika kutimiza ushirikishwaji kikamilifu zipo zitakazotekeleza aina zote mbili za mabaraza (mfano kwa Taasisi zenye Kampasi zinazotumia aina zote mbili za baraza la wafanyakazi ni CBE, OUT, MU) na zipo zitakazotumia baraza la Wafanyakazi pekee (zisizo na kampasi kwa mfano LST, EASTC, WI) ikiwa lengo ni kukidhi mahitaji ya Taasisi husika.

Pamoja na hayo ifahamike kwamba katika Taasisi zenye Kampasi, utofauti wa uendeshaji kati ya Baraza la Wafanyakazi na Baraza Kuu la Wafanyakazi unaonyesha mgawanyo wa majukumu na uwakilishi katika ngazi tofauti ya uendeshaji. Hapa chini ni muhtasari wa tofauti kuu:

### 4.1 Baraza la Wafanyakazi (Campus - Level Council)

i. **Uwakilishi wa Moja kwa Moja:**
   - Linaundwa katika kila kampasi ili kuhakikisha masuala ya eneo husika yanatambuliwa.
   - Wawakilishi huchaguliwa kutoka kwa wafanyakazi wa kampasi husika.

ii. **Majukumu ya Kila Siku:**
   - Kusimamia na kutatua changamoto za kiutendaji na malalamiko ya wafanyakazi ndani ya kampasi.
   - Kupendekeza maboresho ya sera na taratibu kulingana na mazingira ya kazi ya eneo hilo.

iii. **Utoaji wa Mapendekezo ya Moja kwa Moja:**
   - Linahusika katika uamuzi wa masuala ya kiutendaji yanayohusu shughuli za kila kampasi na usimamizi wa rasilimali katika eneo husika.

iv. **Muundo wa Baraza la Wafanyakazi:**

Kwa mujibu wa kanuni ya 25 ya Kanuni za Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2005 (T.S Na. 375) baraza la wafanyakazi litaundwa na wajumbe wafuatao:

i. Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi
ii. Wakuu wa Idara, Kitengo au Sehemu
iii. Wajumbe wa halmashuri ya tawi la Chama cha Wafanyakazi kwenye taasisi husika
iv. Mwakilishi kutoka kila idara, kitengo na Sehemu
v. Mwakilishi kutoka Makao Makuu ya Chama cha Wafanyakazi
vi. Mwakilishi kutoka Baraza Kuu la Wafanyakazi
vii. Afisa anayetekeleza majukumu ya kisheria katika Taasisi husika

## 4.2 Baraza Kuu la Wafanyakazi (Institution - Wide Council)

i. **Uwakilishi wa Kitaasisi:**

- Linahusisha wawakilishi kutoka mabaraza ya kila kampasi, linaloimarisha uwakilishi wa jumla wa wafanyakazi katika Taasisi nzima.
- Linalenga kuunganisha maoni na changamoto kutoka maeneo yote.

ii. **Utangamano wa Sera na Mikakati:**

- Linatengeneza sera na mikakati ya kitaasisi inayolenga kuhakikisha usawa na utoaji wa huduma kwa viwango vya juu.
- Linalofanya kazi kama jukwaa la kuratibu maamuzi ambayo yanaathiri maeneo yote.

iii. **Ushauri na Ulinganifu:**

- Linatoa ushauri kwa uongozi wa Taasisi kuhusu masuala ya ajira na maendeleo ya sera.

- Linasaidia kutatua migogoro au changamoto ambazo hujitokeza kati ya kampasi tofauti, kuhakikisha kuwa maamuzi ya kiutendaji yanayofanywa katika ngazi ya kampasi yanalingana na Sera ya Taasisi nzima.

**iv. Muundo wa baraza Kuu la Wafanyakazi**

Muundo wa **Baraza Kuu la Wafanyakazi** kwa Taasisi zenye kampasi kawaida huzingatia uwakilishi kutoka kwenye kampasi zote ili kuhakikisha ushirikishwaji wa wafanyakazi katika maamuzi. Muundo huu unaweza kutofautiana kulingana na taasisi husika, lakini kwa ujumla unajumuisha:

1. Mwenyekiti wa Baraza (Mkuu wa Taasisi)
2. Katibu wa Baraza
3. Wawakilishi wa Menejimenti ya Taasisi
    - Wakuu wa Idara, Vitengo au Kampasi mbalimbali.
    - Wawakilishi wa ngazi za juu wa menejimenti ili kuwasilisha maoni ya uongozi.
4. Wawakilishi wa Wafanyakazi
    - Wanaweza kuchaguliwa au kuteuliwa kutoka kwenye kampasi zote ili kuhakikisha sauti ya wafanyakazi inasikika.
    - Kwa taasisi kubwa, kunaweza kuwa na uwiano wa idadi ya wawakilishi kulingana na ukubwa wa kampasi au idara.
5. Wawakilishi wa Vyama vya Wafanyakazi
    - Mwakilishi kutoka vyama vya wafanyakazi vinavyotambulika rasmi katika taasisi (Tawi na Taifa)
6. Wawakilishi wa Taasisi ya Serikali

- Katika baadhi ya taasisi, mwakilishi wa Wizara inayosimamia masuala ya kazi anaweza kushiriki kama mgeni au mshauri mathalani Mwakilishi kutoka Ofisi ya Kamishina wa Kazi

7. Mwenyekiti wa Kamati ndogo (Kama zipo)
   - Kamati ya Maadili na Nidhamu.
   - Kamati ya Maslahi na Maendeleo ya Wafanyakazi.
   - Kamati ya Bajeti na Mipango.

### 4.3 Mchakato wa Uundaji wa Mabaraza ya Wafanyakazi

Mchakato wa kuunda mabaraza ya wafanyakazi ni hatua inayohitaji ushirikiano kati ya Chama cha Wafanyakazi, Mwaajiri na mamlaka husika. Hapa chini ni hatua muhimu katika mchakato huu:

**a) Ufuatiliaji wa Sheria na Kanuni**

Kabla ya kuanzisha baraza la wafanyakazi, ni muhimu kufahamu sheria na kanuni zinazohusu haki za wafanyakazi na usimamizi wa mabaraza haya. Nchini Tanzania kama ilivyo kwenye nchi nyingine, kuna Sheria za Kazi (tajwa hapo juu) zinazozungumzia majukumu ya waajiri na wafanyakazi, ikiwa ni pamoja na masharti ya kuanzisha baraza la wafanyakazi.

**b) Ushirikiano na Ridhaa ya Waajiri**

Pamoja na kwamba uanzishaji wa mabaraza ya wafanyakazi ni hitajio la kisheria lakini haliwezi kuanzishwa bila ushirikiano wa waajiri. Waajiri wanapaswa kuelewa faida ya kuwa na baraza la wafanyakazi, ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kazi, kuongeza uzalishaji, na kupunguza migogoro kazini. Mara nyingi, mabaraza haya huanzishwa baada ya mazungumzo kati ya Chama cha Wafanyakazi na waajiri.

**c) Kuandaa Mkataba wa kuunda wa Baraza la Wafanyakazi**

Baraza la wafanyakazi kwenye taasisi husiaka linahitaji kuwa na mkataba unaosimamia utendaji wake. Mkataba huo unapaswa kuainisha muundo wa baraza, majukumu ya baraza pamoja na wajumbe, utaratibu vikao, na jinsi ya kutatua migogoro inayojitokeza. Hii ni muhimu ili kuhakikisha kuwa baraza linaendeshwa kwa uwazi na ufanisi kwa kuzingatia Sheria.

**d) Uchaguzi wa Wajumbe wa Baraza**

Mabaraza ya wafanyakazi yanapaswa kuwa na wawakilishi kutoka kwa wafanyakazi ambao wamechaguliwa kwa njia ya kidemokrasia. Uchaguzi wa wajumbe unapaswa kufanyika kwa uwazi, na wafanyakazi wanapaswa kuwa na haki ya kuchagua wawakilishi wao. Kila mhusika anapaswa kuwakilishwa kwa usawa. Kwa utaratibu zoezi la uchaguzi wa wawakilishi kutoka idara huwa linasimamiwa na mtaalamu kutoka ofisi ya Kamishina wa Kazi.

**e) Kufanya Vikao kwa Mujibu wa Mkataba**

Mabaraza ya wafanyakazi yanapaswa kufanya vikao vya mara kwa mara ili kujadili masuala muhimu kulingana na ratiba iliyoainishwa kwenye Mkataba. Kwa mujibu wa sheria, baraza la Wafanyakazi linatakiwa kufanyika mara mbili kwa mwaka na endapo itatokea dharura litaitishwa baraza la dharura kujadili suala hilo.

## 4.4 Utaratibu wa kuunda Mabaraza ya Wafanyakazi Mahala Pa kazi kwenye Vyama Viwili vya Wafanyakazi

Uanzishaji wa baraza la Wafanyakazi ni jambo la kisheria ambapo utekelezaji wake unapaswa kuzingatia misingi ya kisheria kwa kufuata utaratibu ulioanishwa katika miongozo husika. Ni suala lililowazi kwamba kwa mujibu wa kifungu cha 73(1) Cha sheria ya ajira na mahusiano kazi sura 366 kinasema ***"Chama cha wafanyakazi kinachotambuliwa na mwajiri au jumuiya ya waajiri wanaweza kuhitimisha***

***makubaliano ya pamoja kuanzisha Baraza la wafanyakazi kwa ajili ya wafanyakazi kushiriki katika eneo la kazi"***

Kwa kuzingatia maelekezo hayo Mabaraza ya Wafanyakazi yalikuwa yanaundwa na Chama kimoja (kinachotambuliwa) kwani kutambuliwa kwa Chama kwa tafsiri ya kisheria kumeelezwa katika kifungu cha 67 cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini kama ifuatavyo:

***"Chama cha wafanyakazi kilichosajiliwa kinachowakilisha waajiriwa wengi katika kitengo husika cha majadiliano kitakuwa na haki ya kutambuliwa kama wakala pekee wa majadiliano wa Wafanyakazi katika kitengo hicho"***

Katika hali hiyo, miaka ya nyuma uundaji wa mabaraza ya Wafanyakazi mahala pa kazi ulikuwa unafanyika baina ya Chama cha Wafanyakazi (Kinachotambuliwa) pamoja na Menejimenti ya Taasisi hadi pale yalipotoka maelekezo kutoka mamlaka inayosimamia na kusaidi masula ya mabaraza ya wafanyakazi mahala pa kazi (Ofisi ya Kamishna wa Kazi) kwamba uwepo wa mabaraza ya wafanyakazi umetokana na dhana na misingi ya wafanyakazi kupewa fursa ya kushirikishwa na kushiriki katika mambo muhimu ya Taasisi.

Kwa hiyo, kwa kuzingatia uhalisia huo na kuepuka kukiuka lengo la Wafanyakazi kushirikishwa bila kusahau kuepuka uvunjaji wa Sheria ilielekezwa mabaraza ya Wafanyakzi kuundwa na Vyama vyote vilivyopo sehemu ya kazi pamoja na menejimenti ya Tasisi, kwani kutoshirikisha Chama kingine kilichopo mahala pa kazi inaakisi suala la ubaguzi kwa Chama cha Wafanyakazi kushirikishwa kuunda baraza la Wafanyakazi kupitia kifungu cha 8 (1) ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Sura 366.

Kuanzia hapo utekelezaji wa mabaraza mseto (Vyama Viwili vya Wafanyakazi na Menejimenti ya taasisi) ulianza mathalani THTU ilifanikiwa kuunda mabaraza ya namna hiyo na Chama kingine (RAAWU) katika baadhi ya Taasisi ikiwemo MNMA, NIT, TEWW – DSM, UDSM, DIT – KAMPASI KUU, NIT, EASTC n.k

### 4.4.1 Muundo wa Baraza Mseto (Vyama Viwili na Menejimenti ya Taasisi)

Maeneo mengine ya muundo wa baraza la Wafanyakzi unabakia kama ulivyo kwenye Kanuni isipokuwa kwenye wajumbe wa Vyama vya Wafanyakazi (Halmashauri ya Vyama na Wawakilishi kutoka Kanda/Taifa) itakuwa kama ifuatavyo:

i. Wajumbe wa halmashuri ya tawi la Chama cha Wafanyakazi kwenye Taasisi husika:

Kutokana na baadhi ya maeneo ya kazi kuwa na Vyama zaidi ya kimoja, utaratibu unaotumika kubainisha kundi hili la wajumbe ni Vyama vilivyopo kutoa idadi ya wajumbe kwa uwiano kulingana na ukubwa wa uwakilishi (Wingi wa Wanachama). Kwa uzoefu uwiano huo huwa ni 1:3 ya wajumbe wa Halmashauri ya Tawi. Kwa maana nyingine ni kwamba Chama chenye wanachama wengi kitakuwa na uwakilishi mkubwa kuliko Chama chenye Wanachama Wachache. Hata hivyo, hakuna Sheria au Kanuni maalum iliyoelekeza moja kwa moja kuhusu uwiano wa mgawanyo wa wajumbe pale inapotokea baraza linaundwa na Chama zaidi ya kimoja hali ambayo inatupasa kuendelea kuzingatia uwiano wa Wawakilishi wa Chama uliobainishwa katika kifungu cha 62 (1) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Sura 366 wakati zoezi la majadiliano ya uwiano wa uwakilishi linapofanyika.

ii. Mwakilishi kutoka Makao Makuu ya Chama cha Wafanyakazi

- Kila Chama kinatawikiwa kutoa mwakilishi mmoja kutoka Makao Makuu ya Chama.

Kwa hiyo, katika suala la uundaji wa baraza la wafanyakazi lenye vyama viwili, sehemu inayoathirika na mabadiliko ni muundo wa baraza husika ukilinganisha na baraza linaloundwa na Chama kimoja. Utaratibu wa sehemu nyingine unabaki kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria na Kanuni.

### 4.4.2 Changamoto za mabaraza yanaundwa na Vyama Viliwili vya Wafanyakazi

i. Undaji wa mabaraza ya namna hii unachangamoto hususani kwenye hatua za awali za maandalizi ya mkataba, kwani endapo ikitokea pande hazina uelewa vizuri wa kupata uwiano wa wajumbe kutoka katika Halmshauri za matawi huwa inaleta marumbano yasiyo na tija.

ii. Uundwaji wa Mabaraza yanayojumuisha Vyama vyote vilivyopo ndani ya taasisi yanaleta mantiki kwenye dhana ya ushirikishwaji mahala pa kazi, lakini suala hili halijawekwa vizuri kwenye miongozo ya Sheria zilizoanzaisha mabaraza ya Wafanyakazi hali inayoleta sintofahamu kwenye baadhi ya nyakati wakati wa utekelezaji wa suala hili.

iii. Migongano ya Maslahi: Vyama tofauti vinaweza kuwa na malengo au mikakati inayotofautiana, hali inayoweza kusababisha migongano katika maamuzi ya baraza.

iv. Ugumu katika kufikia maamuzi, hali ya tofauti za kiitikadi na kimuundo kati ya vyama zinaweza kufanya mchakato wa maamuzi kuwa mgumu na wa polepole, hivyo kuathiri ufanisi wa baraza.

## 4.5 Orodha ya matawi ya THTU yenye Mabaraza ya Wafanyakazi/Baraza Kuu la Wafanyakazi

| Na. | JINA LA TAASISI | BARAZA LA WAFANYAKAZI | BARAZA KUU LA WAFANYAKAZI |
|---|---|---|---|
| 1. | CHUO CHA MIPANGO YA MAENDELEO VIJIJINI (IRDP), DODOMA | √ | |
| 2. | CHUO CHA MIPANGO YA MAENDELEO VIJIJINI, KANDA YA ZIWA (IRDP) KAMPASI YA MWANZA | | |
| 3. | CHUO CHA SERIKALI ZA MITAA, HOMBOLO (LGTI) | √ | |
| 4. | TAASISI YA USTAWI WA JAMII (ISW) | √ | |
| 5. | TAASISI YA USTAWI WA JAMII (ISW) KAMPASI YA KISANGARA | | |
| 6. | CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE (MNMA) | √ | |
| 7. | TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA (TEWW), DAR ES SALAAM | √ | |
| 8. | TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA (TEWW), KAMPASI YA MWANZA | | |
| 9. | CHUO CHA TAIFA CHA USAFIRISHAJI (NIT) | √ | |

| Na. | JINA LA TAASISI | BARAZA LA WAFANYAKAZI | BARAZA KUU LA WAFANYAKAZI |
|---|---|---|---|
| 10. | MAMLAKA YA ELIMU TANZANIA (TEA) | √ | |
| 11. | CHUO CHA UHIFADHI NA USIMAMIZI WA WANYAMA PORI (CAWM), MWEKA | √ | |
| 12. | CHUO CHA MAENDELEO YA JAMII TENGERU (TICD) | √ | |
| 13. | CHUO KIKUU CHA USHIRIKA MOSHI (MoCU) | √ | |
| 14. | CHUO KIKUU CHA USHIRIKA MOSHI (MoCU), KAMPASI YA KIZUMBI, SHINYANGA | | |
| 15. | CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA ELIMU MKWAWA (MUCE) | √ | |
| 16. | CHUO CHA ELIMU YA BIASHARA (CBE), DAR ES SALAAM | √ | √ |
| 17. | CHUO CHA ELIMU YA BIASHARA (CBE)- DODOMA KAMPASI | √ | |
| 18. | CHUO CHA ELIMU YA BIASHARA (CBE) - MBEYA KAMPASI | √ | |
| 19. | CHUO CHA ELIMU YA BIASHARA (CBE) - MWANZA KAMPASI | √ | |
| 20. | CHUO KIKUU CHA ARDHI (ARU) | √ | |
| 21. | TAASISI YA MAENDELEO YA USIMAMIZI WA MAJI (WI) | √ | |
| 22. | CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM (UDSM) | √ | |
| 23. | TAASISI YA AFRIKA YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA YA NELSON MANDELA (NM- AIST) | √ | |
| 24. | CHUO CHA UFUNDI ARUSHA (ATC) | √ | |
| 25. | TAASISI YA MAFUNZO YA UANASHERIA KWA VITENDO TANZANIA (LST) | √ | |
| 26. | CHUO KIKUU CHA DODOMA (UDOM) | √ | |
| 27. | TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA (TCU) | √ | |
| 28. | TAASISI YA ELIMU TANZANIA (TET) | √ | |
| 29. | CHUO KIKUU MZUMBE (MU), MOROGORO | √ | √ |
| 30. | CHUO KIKUU MZUMBE (MU), KAMPASI YA MBEYA | √ | |
| 31. | CHUO KIKUU MZUMBE (MU), KAMPASI YA DAR ES SALAAM | | |
| 32. | CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA ELIMU DAR ES SALAAM (DUCE) | √ | |
| 33. | CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO (SUA), MOROGORO | √ | |
| 34. | CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO (SUA) KAMPASI YA MIZENGO | | |

| Na. | JINA LA TAASISI | BARAZA LA WAFANYAKAZI | BARAZA KUU LA WAFANYAKAZI |
|---|---|---|---|
| | PINDA (MPC) | | |
| 35. | CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA (OUT) | √ | √ |
| 36. | CHUO KIKUU CHA SAYANSI NA TEKNOLOGIA MBEYA (MUST) | √ | |
| 37. | CHUO CHA UHASIBU ARUSHA (IAA) | √ | |
| 38. | CHUO CHA TAKWIMU MASHARIKI MWA AFRIKA (EASTC) | √ | |
| 39. | TAASISI YA TEKNOLOGIA DAR ES SALAAM (DIT) | √ | |
| 40. | TAASISI YA TEKNOLOGIA DAR ES SALAAM (DIT) KAMPASI YA MWANZA | | |
| 41. | CHUO KIKUU CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI MUHIMBILI (MUHAS) | √ | |
| 42. | CHUO KIKUU CHA TUMAINI DAR ES SALAAM (DarTU) | √ | |
| 43. | CHUO KIKUU CHA UMOJA WA AFRIKA TANZANIA (UAUT) | | |
| 44. | CHUO KIKUU CHA ST. JOHN TANZANIA (SJUT) | | |
| 45. | CHUO KIKUU KISHIRIKI MARIAN (MARUCo) | | |
| 46. | CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA JORDAN (JUCo) | | |
| 47. | CHUO KIKUU TEOFILE KISANJI (TEKU) | | |
| 48. | CHUO KIKUU CHA MWANZA (MzU) | | |
| 49. | BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (NACTVET) | | |
| 50. | CHUO KIKUU CHA KILIMO NA TEKNOLOJIA CHA MWALIMU JULIUS K. NYERERE (MJNUAT) | | |
| 51. | CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA STELLA MARIS MTWARA (STEMMUCo) | | |
| | **JUMLA KUU** | **35** | **3** |

## 4.6 Matawi yanayopaswa kuwa na Baraza Kuu la Wafanyakazi

Katika orodha ya matawi tajwa hapo juu zipo baadhi ya Taasisi zinapaswa kuwa na Baraza Kuu la Wafanyakazi (Master Workers Council) kulingana na ukubwa wa Taasisi hizo kuwa na Kampasi, lakini labda kutokana na Menejimenti kutokuwa na uelewa mzuri kuhusu suala la uendeshaji wa mabaraza ya Wafanyakazi, Taasisi husika hazina baraza kuu la Wafanyakazi, miongoni mwa Taasisi hizo ni pamoja na DIT, IRDP, SUA, MoCU.

Ikimbukwe kwa Baraza la Wafanyakazi linaanzishwa sehemu ya kazi yenye Watumishi kuanzia kumi (10) na kuendelea kama ilivyoelekezwa kwenye agizo la Rais Na. 1 la mwaka 1970. Katika hali hiyo, zipo Taasisi zenye kampasi ambazo hazina Mabaraza ya Wafanyakazi licha ya kampasi hizo kuwa na idadi ya Watumishi inayokidhi takwa na kuunda baraza la Wafanyakazi katika eneo hilo la Kazi, miongoni mwa Taasisi hizo ni pamoja na DIT – Kampasi ya Mwanza, IRDP Kampasi ya Mwanza, SUA – MPC n.k, Hali hiyo ni ukiukwaji wa miongozo ya uundwaji wa mabaraza sehemu za kazi.

### 4.6.1 Ushauri na Mapendekezo

Taasisi zote zenye Kampasi ambazo zimekidhi takwa la kuwa na Watumshi kumi na kuendelea zinatakiwa kuanzisha baraza la Wafanyakazi katika Taasisi husika ili kutoa fursa ya ushirikishwaji wa wafanyakazi wanaofanyakazi katika eneo husika, kisha kuunda Baraza Kuu la Wafanyakazi ambalo litakuwa lianundwa na wajumbe kutoka kampasi zote.

## 4.7 Kazi/Majukumu za Baraza la Wafanyakazi

Kazi za baraza la wafanyakazi zitakuwa kama ifuatavyo: -

i. Kushauri Uongozi wa Chuo katika maswala yote yahusuyo upandishwaji wa vyeo na masuala ya nidhamu katika utumishi wa umma.
ii. Kushauri Menejimenti ya Taasisi juu ya hatua zinazopaswa kuchukuliwa katika utoaji wa huduma bora, ili kujenga uchumi thabiti kwa Taifa.
iii. Kushauri Menejimenti ya Taasisi katika masuala yahusuyo watumishi, pamoja na maslahi yao katika utumishi wa umma.
iv. Kushauri Menejimenti ya Taasisi kuhusiana na mabadiliko ya sheria, kanuni na miongozo mbalimbali inayohusu mazingira ya utumishi.
v. Kujadili na kushauri masuala yahusuyo mipango ya Taasisi, mapato na matumizi yake

vi. Kujadili na kutoa ushauri kuhusu masuala yahusuyo mafunzo na maendeleo ya wafanyakazi.

vii. Kukuza ushirikiano kati ya wafanyakaza na Menejimenti ya Taasisi katika kuwezesha shughuli za serikali.

viii. Kujadili na kutoa mapendekezo ya ushiriki wa Taasisi katika huduma za kijamii.

## 5. CHANGAMOTO YA UENDESHAJI WA MABARAZA YA WAFANYAKAZI

### i. Upinzani kutoka kwa Waajiri

Katika baadhi ya Taasisi, Waajiri wanaweza kuona uundaji wa baraza la Wafanyakazi kama changamoto kwa usimamizi wao, hivyo wanajitahidi kupinga mchakato huu. Hii inaweza kutokea kutokana na hofu ya kupoteza udhibiti au kupandisha gharama za uendeshaji.

### ii. Upungufu wa Ufahamu

Wafanyakazi wengi hawana elimu ya kutosha kuhusu umuhimu na manufaa ya mabaraza ya wafanyakazi. Hii inaweza kuathiri ushiriki wao katika mchakato wa uchaguzi wa wajumbe au utekelezaji wa majukumu ya baraza.

### iii. Kutokuelewana kuhusu majukumu ya Baraza

Mara nyingine, wafanyakazi na waajiri wanaweza kutokuelewana kuhusu majukumu na haki za baraza. Hii inaweza kuleta migogoro au kutofautiana katika utekelezaji wa mipango au mapendekezo ya baraza.

## 6. MAPENDEKEZO YA UTATUZI WA CHANGAMOTO YA UUNDAJI WA MABARAZA YA WAFANYAKAZI

Changamoto za uundaji wa mabaraza ya wafanyakazi zinaweza kuwa nyingi, lakini kuna mapendekezo mbalimbali ya kuzitatua ili kuhakikisha kuwa mabaraza haya yanaanzishwa na kufanya kazi kwa ufanisi. Hapa kuna baadhi ya mapendekezo muhimu:

### ii. Kutoa Elimu ya Mabaraza ya Wafanyakazi

Kwa utaratibu suala la uwezeshaji wa elimu kuhusiana na baraza ya wafanyakazi lipo chini ya Ofisi ya Kamishina wa Kazi lakini Chama cha Wafanyakazi tunalo jukumu la kuandaa semina na warsha kwa wafanyakazi kuhusu:

- Umuhimu wa mabaraza ya wafanyakazi.
- Sheria na kanuni zinazosimamia uanzishwaji wa mabaraza haya.
- Haki na wajibu wao ndani ya baraza.

### iii. Kuimarisha Mfumo wa Kisheria na Kiusimamizi

Serikali kupitia ofisi ya Kamishna wa Kazi ihakikishe kuwa sheria zinazoongoza uundaji wa mabaraza haya zinatekelezwa kikamilifu. Ikiwa pamoja na kuchukua hatua kwa waajiri wanaopinga au kuchelewesha uundaji wa mabaraza haya.

### iv. Ushirikiano kati ya Waajiri na Wafanyakazi

Ni wakati wa kuhamasisha waajiri kuona mabaraza haya kama njia ya kuboresha uzalishaji na sio tishio kwao.

## 7. HITIMISHO

Uundaji wa mabaraza ya wafanyakazi ni hatua muhimu katika kuboresha mazingira ya kazi, kuhakikisha usawa kazini pamoja na kuongeza tija. Ingawa kuna changamoto zinazoweza kutokea, faida za mabaraza haya ni nyingi na zinasaidia pande zote (Wafanyakazi, Waajiri, na jamii kwa ujumla). Ili mabaraza haya yawe na ufanisi, ni muhimu kwa wafanyakazi, waajiri, na serikali kushirikiana katika kutekeleza mchakato huu kwa ufanisi.

## 8. REJEA


i. Agizo la Rais Namba 1 la mwaka 1970
ii. Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Sura 366
iii. Sheria ya Majadiliano ya pamoja katika Utumishi wa Umma Sura 105
iv. Kanuni za Majadiliano ya pamoja katika Utumishi wa Umma za mwaka 2003 (T.S. Na. 19)
v. Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298
vi. Kanuni Za Utumishi wa Umma za mwaka 2022 (T.S. Na. 444).